MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO



*Na.27: Msimu wa Kilimo 2025/26* *Tathmini ya June 21-30, 2026 na Matazamio kwa Kipindi cha Julai 1-10, 2026*

**MUHTASARI**

- Mvua zinazotarajiwa katika maeneo machache yanayopata misimu miwili kwa mwaka zitaendelea kusaidia ukuaji wa mazao yaliyochelewa kupandwa na upatikanaji wa malisho kwa ajili ya mifugo
- Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo yanayopata msimu mmoja kwa mwaka itasaidia katika ukaushaji, kukomaa kwa mazao mashambani na shuguli za uvunaji
- Wakulima wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.


## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilisababisha ukanda mvua kuendelea kusogea kuelekea kaskazini zaidi nje ya nchi yetu. Vilevile, upepo wa bahari wenye unyevunyevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani uliimarisha kwa vipindi mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani hususan yale yaliyopo nyanda za juu kaskazini mashariki.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vya mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na yale ya nyanda za juu kaskazini mashariki.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2026

Katika dikadi hii, maeneo mengi nchini yalikuwa makavu isipokuwa katika maeneo machache ya mkoa wa Kilimanjaro yalipata mvua ya siku kumi kiasi cha milimita 26 hadi 100 kama inavyooneshwa katika Kielelezo.




*Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha June 21-30, 2026*

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-302026

Katika dikadi hii, kiasi cha mvua kilichorekodiwa katika ma neo mengi ya nchi kilipungua kiasi. Licha ya upungufu huo, unyevunyevu katika udongo kwa ujumla ulibakia kuwa mzuri katika maeneo mengi. Katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hali hii ilisaidia ukuaji wa mazao. Hata hivyo, hali ya ukavu uliojitokeza zaidi katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka ulisaidia katika ukaushaji na ukomavu wa mazao na pia katika shughuli za uvunaji.

Katika maeneo yenye misimu miwili ya mvua, zao la mahindi lilikuwa katika hatua za kuanza kukomaa, hasusan katika bonde la Ziwa Victoria na Pwani ya Kaskazini na wakulima katika maeneo haya waliendelea na shughuli za kawaida za usimamizi wa mazao mashambani.

Zao la mpunga katika mkoa wa Morogoro lilikuwa katika hatua ya maziwa hadi ubichi laini. Wakati huohuo, katika mikoa ya Mwanza, Mbeya na Rukwa, Tabora, na Shinyanga, zao hilo lilikuwa tayari kuvunwa na wakulima waliendelea na shughuli za uvunaji wa zao hilo. Pia zao la alizeti liko katika hatua ya kukomaa katika miikoa ya Dodoma,Morogpro na Singida.

Kwa upande wa mazao ya kudumu, zao la kahawa katika mikoa ya Kilimanjaro na Songwe ilikuwa katika hatua ya kujaza matunda. Kwa upande mwingine, karafuu katika Visiwa vya Pemba zilikuwa katika hatua yya karafuu changa na wakulima wakijikita katika ufuatiliaji wa wadudu na magonjwa mashambani.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo na wanyamapori umeanza kupungua kutokana na hali ya ukavu iliyojitokeza.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2026

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kimepungu kidogo kutokanana na hali ya ukavu inayoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2026

Katika dikadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kudhohofika.

Hali hii inatarajiwa kudumisha mwenendo wa ukandamvua kuelekea kaskazini zaidi, nje ya nchi yetu. Vilevile, upepo wa bahari wenye unyevunyevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani unatarajiwa kuimarisha kwa vipindi mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani hususan yale yaliyopo nyanda za juu kaskazini mashariki

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2026

Maeneo kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi), kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kupata hali ya ukavu kwa ujumla.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) kunatarajiwa kupata vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida) yanatarajiwa kupata hali ya ukavu. Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) kunatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2026

Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi nchini inayotarajiwa itasaidia katika kukomaa, kuvuna , kukauka na uhifadhi wa mazao maghalani.

**USHAURI**

- **Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (bonde la Ziwa Victoria, nyanda za juu za kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini):** Wakulima wanashauriwa kufuatilia utabiri wa hali ya hewa wa kila siku na kujiandaa na mvua za muda mfupi katika maeneo machache, ili kupanga shughuli za kilimo kwa wakati unaofaa, kama vile kupulizia dawa za wadudu pale inapobidi.

- **Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (pwani ya kusini, maeneo ya magharibi, maeneo ya kati, nyanda za juu za kusini magharibi na maeneo ya kusini):** Wakulima wanashauriwa kuendelea kufuatilia ukuaji wa mazao katika hali ya ukavu; Alizeti katika mkoa wa Dodoma na Singida, ambayo iko katika hatua ya kukomaa inapaswa kufuatiliwa dhidi ya uharibifu unaosababishwa na ndege na kuvunwa mara tu mbegu zinapokomaa.

  **Wavuvi wanaotumia Bahari kuu na Maziwa makubwa:** Wanashauriwa kuendelea kufuata utabiri wa hali ya hewa wa kila siku, hasa wakati wa upepo mkali na mawimbi makuu, na kupanga safari fupi za uvuvi, kukaa karibu na bandari salama wakati wa nyua za radi zinazotarajiwa.

Ushauri huu unalenga kuongeza tija ya kilimo na kupunguza hatari zinazohusiana na hali mbaya ya hewa. Wakulima na wadau wa kilimo wanashauriwa kutumia taarifa za hali ya hewa kwa ufanisi na kushauriana na maafisa ugani wa kilimo ili kupanga shughuli za kilimo vyema zaidi.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2026

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kupungua kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa. Jamii inashauriwa kuhifadhi maji kwa ajili ya matumizi ya baadae.